

Maswali

1. Mfalme Nebukadreza alitengeneza nini?
2. Watu wangepanya nini wakisikia muziki?
3. Nini ingefanyika kwa mtu aliyekataa kuisujudia?
4. Nani hangeisujudia?
5. Watu wa hiyo nchi walimwambia nini Mfalme?
6. Shadraka, Meshaki na Abednego walimwambia nini Mfalme?
7. Tanuru ilifanywa moto mara ngapi zaidi?
8. Nini ilifanyika kwa wale watu waliowatupa kwa tanuru?
9. Nebukadreza aliona watu wangapi kwa tanuru?
10. Nani aliwaita watoke ndani ya tanuru?

Majibu

1. Mfalme Nebukadreza alitengeneza sanamu ya dhahabu.
2. Watu wangepanya muziki wakisikia muziki.
3. Angetupwa ndani ya tanuru ya moto.
4. Shadraka, Meshaki na Abednego hawakuisujudia.
5. Watu walimwambia kwamba Shadraka, Meshaki na Abednego hawakuisujudia.
6. Shadraka, Meshaki na Abednego walisema eti Mungu angewaokoa.
7. Tanuru ilifanyika moto mara saba zaidi.
8. Watu waliowatupa ndani walikufa.
9. Nebukadreza aliona watu wanne ndani ya tanuru.
10. Mfalme Nebukadreza aliwaita watoke nje ya tanuru.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

32 Tanuru ya moto

Marejeo

Danieli 3

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu huokoa wamwaminio

Maneno maalum

1. Mfalme + sanamu ya bhahabu + kusujudia + tanuru.
2. Tii + Shadraka, Meshaki na Abednego wakataa.
3. Mfalme + kasirika + kusujudia + abudu Mungu wa Binguni + anaokoa.
4. Mfalme Nebukadreza + moto mara 7 + watu wanne + toka nje.
5. Kutochomeka + hakuna harufu ya moto + barikiwa + Malaika.

32.1 Mfalme Nebukadreza alitengeneza sanamu kubwa sana ya dhahabu. Ingeonekana kutoka mbali kwa ajili ya ukubwa wake. Aliwaambia watu wote waisujudie wanaposikia muziki ikichezwa. Yeyote atakayekataa kuisujudia angetupwa ndani ya tanuru [moto kali sana]. Watu wote katika ufalme wa Nebukadreza waliisujudia waliposia muziki. Lakini kulikuwa na marafiki watatu wayahudi hawakuisujudia hiyo sanamu ya dhahabu kwa sababu walimpenda Mungu. Muziki ulipochezwa watu wote waliinama chini kusujudia lakini hao walisimama tu.

32.2 Baadhi ya watu wa nchi hiyo walienda kumuona Mfalme Nebukadreza na kumwambia juu ya hao marafiki watatu-Shadraka, Meshaki na Abednego. Walisema, “Hawa watu hawaja kutii wewe, Ee Mfalme. Hawasujudii hiyo sanamu ya dhahabu uliyoitengeneza.”

32.3 Mfalme alikasirika sana, akasema, “Leta hao watu Shadraka, Meshaki na Abednego,” waliletwa kwa Mfalme. Akawauliza, “Eti nyinyi Shadraka, Meshaki na Abednego mmekataa kuisujudia sanamu ya dhahabu niliyoitengeneza? Mkisikia sauti ya muziki lazima muisujudie sanamu ya dhahabu la sivyo mtatupwa ndani ya tanuru iwakaayo.” Shadraka, Meshaki na Abednego wakamwangualia mfalme aliyekuwa na hasira na kusema, “Sisi tunamwabudu Mungu wa kweli, Mungu wa Mbinguni, hatuabudu miungu yako. Hatutasujudia sanamu yako ya dhahabu. Ukitutupa ndani ya tanuru ya moto, Mungu wetu anaweza kutuokoa kutoka kwa moto.”

32.4 Mfalme Nebukadreza alighadhabika na kutoa sauti. “Tanuru iwekwe moto mara 7 zaidi ya kawaida. Agiza watu kutoka kwa jeshi langu walio na nguvu wawafunge hawa watatu na kutupwa kwa tanuru ya moto.”

Kwa hivyo wakawafunga Shadraka, Meshaki na Abednego wakawatupa ndani ya tanuru ya moto wakiwa bado wamevaa makoti, suruali na kofia. Tanuru ilikuwa moto zaidi kwa hivyo ikachoma na kuua wale watu waliowatupa. Mfalme aliangualia wakati walipotupwa kwa tanuru. Akaangualia kwa mshangao. Akasema, “Tulitupa watu watatu motoni lakini nawaona watu wanne katikati ya moto hawajaumia, wa nne anaonekana ni kama malaika.” Kwa hivyo aliita, “Shadraka, Meshaki na Abednego, watumisha wa Mungu Mkuu toka nje ya tanuru.”



32.5 Shadraka, Meshaki na Abednego walitoka nje ya tanuru na kusimama mbele ya Mfalme. Hawakuwa wamechomeka wala nguo zao hazikuwa na harufu ya moto. Nebukadreza alisema, “Abarikiwe Mungu wa Shadraka, Meshaki na Abednego wanaemwamini aliyetuma malaika awaokoe watumishi wake.” Mfalme aliwafanya Shadraka, Meshaki na Abednego wawe watu wa maana kwa ufalme wake.